



## UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Kiango (2002), dhima kuu ya lugha yoyote ni kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii ya watu walio na utamaduni sawa. Aidha, lugha hutumika pia kama kitambulisho cha jamii fulani na vilevile kama njia mojawapo ya kuelezea na kuhifadhi utamaduni wake. Hata hivyo, baaadhi ya watafiti kama vile Seargeant na Earling (2011) wanaeleza kwamba lugha yafaa ichukue nafasi kubwa katika maendeleo ya kijamii licha ya lugha yenyewe kubeba utamaduni na kutumika katika mawasiliano ya jamii. Katika jamii, lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano. kama jamii nyingine duniani, jamii ya Afrika mashariki inajivunia lugha ya Kiswahili kama nyenzo mojawapo ya mawasiliano katika mataifa mengi ya Afrika mashariki. Lugha nyingine zinazozungumzwa Afrika mashariki kando na lugha-mame za wazaliwa wa Afrika mashariki ni, Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani. Lugha hizi zilizokuja na mkoloni pia zimepata nafasi kubwa katika jamii ya Afrika kwa ujumla. Siku za hivi karibuni kumeshuhudiwa ongezeko la matumizi ya lugha ya Kichina na mafunzo kutolewa kwa waafrika kwa lugha hii. Hata hivyo, lugha hizi zinaendelezwa kwa mtazamo na imani za waafrika wenyewe. Waafrika wengi wanaamini kuwa, maendeleo na kungeuka kunatokana na lugha hizi za kikoloni. Mitazamo hii ni tata na imelifanya bara la Afrika kuyumba kimaendeleo. Maendeleo huanza kupitia kwa mawasiliano ambapo mawasiliano hayo hudhibitiwa na lugha ya wazungumzaji. Kupitia lugha hizi za kigeni basi, kuna mkachanganyiko na hivyo kulemaza mawasiliano katika jamii ya Afrika. Lugha kama zao la kijamii huleta umoja miongoni mwa wanajamii kutokana na kule kuelewana katika matumizi ya istilahi pamoja na utamaduni sawa. Kuwepo kwa lugha nyingi za kigeni na ambazo zinashabikiwa sana na waafrika, kumedumaza mawasiliano na hivyo kurejesha nyuma maendeleo.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Utafiti huu unaangazia baadhi ya tafiti zilizofanywa kuhusiana na matumizi ya wingi lugha na inavyoathiri uchumi na pia kuangazia matumizi ya lugha moja na namna inavyoathiri uchumi. Mwisho tutahusisha tafiti hizi za awali na namna Kiswahili kinakuza maendeleo ya jamii kiuchumi. Mwanzo, tutaangazia namna wingi lugha huathiri maendeleo ya jamii. Watafiti Easterly na

Levine (1997), Lian na Oneal (1997), Alesina na La Ferrara (2005) katika tafiti zao wanabaini kwamba, wingi lugha hurejesha nyuma maendeleo ya jamii. Watafiti hawa wanafikia uamuzi huu kutokana na hoja kwamba, wingi lugha huchangia vita baina ya koo zilizona tamaduni tofauti. Aidha, wingi lugha hupunguza uaminifu baina ya jamii hizi zenye tamaduni tofauti na hivyo kuchangia kuwepo kwa mfumo dhabiti wa kisiasa na kuchumi kutoka kwa jamii inayoonekana kustawi Zaidi. Noguier na Siscart (2003) wanahoji kwamba, kikwazo katika lugha au kufanya biashara na mtu ambaye hamwelewani katika lugha, mara nyingi hutatiza biashara hiyo aidha kuwa finyu au isiendele kabisa. Hata hivyo, watafiti katika uwanja wa ujifunzaji wa lugha ya pili kama vile Ku na Zussman (2008) wanasema kwamba, kikwazo hiki cha kimawasiliano kinaweza kuondolewa na ujifunzaji wa lugha za kigeni kwa mwenyeji anayetaka kufanya biashara na watu wa mataifa mengine.

Bibilia takatifu miongoni mwa Wakristu pia inatambua umuhimu wa lugha moja katika maendeleo ya jamii. Katika kitabu cha Mwanzo 11:5-7; “Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. Bwana akasema, “Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuliwa neno wanalokusudia kulifanya. Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao”. Basi Bwana akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji.” Katika nukuu hii tunatambua kwamba lugha ilitumika kama kiunganishi cha watu wa jamii na taifa hili ndipo wakaweza kujenga mnara kwa kima kirefu kama kile. Na ili wasifaulu katika safari ya ujenzi Mungu aliwatawanya katika lugha mbalimbali na hivyo wakakosa maelewano baina yao. Ujenzi wa mnara haukuendelea tena, kila mmoja alishika njia na kwenda zake kwa kukosa malengo au maono sawa. Hii inatuonyesha nini? Kwamba, kwa kukosa lugha moja ambayo inaweza kuunganisha jamii au taifa au bara, maendeleo au maono huenda yasiweze kuafikiwa kwa pamoja kwani kila mmoja atajaribu kuvuta upande wake.

Mkwinda (2014) anaeleza kuwa lugha ni nyenzo ya kustawisha uchumi wa kijamii. Katika kutetea hoja

yake anasema kwamba, kuna umoja katika matumizi ya lugha moja na pia kuna nguvu katika matumizi ya lugha moja katika taifa eneo fulani la kijeografia. Hivyo, ili kuwepo na maendeleo madhubuti katika eneo fulani, muhimu si lugha bali mawasiliano bora na mwishowe mawasiliano hayo huleta umoja. Hivyo, umoja wa taifa au jamii huimarika kupitia kwa matumizi ya lugha ambayo ni sawa na inazungumzwa na watu fulani katika eneo lao. Kila mtu katika eneo hili hutaka kujinasibisha na mwenzake mwenye lugha sawa na kujitofautisha na wengine wasio na lugha sawa na wao. Kwa mfano, nchini Malawi, katika kutoa vipande kwa wananchi wao, walitoa vipande hivyo kwa kuzingatia lafudhi ya Wamalawi na kuwanyima wale ambao hawakuwa na lafudhi sawa na Wamalawi. Hii ilitokana na dhana kwamba, rangi ya ngozi haiwezi kutumika kutenga mtu ila lugha.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Juhudi za Kupanua Matumizi ya Kiswahili Afrika

Makala haya yanatilia mkazo wazo kwamba ili kuwepo na maendeleo dhabiti na endelevu ya kiuchumi, mawasiliano bora yanafaa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Maendeleo huanza na mtu mmoja, kisha familia, jamii na kisha taifa nzima. Uwezekano wa maendeleo unategemea lugha na mawasiliano bora kutoka kwa mtu binafsi. Nchi za Afrika na pia mataifa wanachama wa muungano wa Afrika Mashariki, mawasiliano yamekuwa kikwazo katika maendeleo ya kiuchumi. Nchi hizi zimeshindwa kustawisha uchumi kupitia biashara miongoni mwao kwa kukosa mawasiliano. Conway (1994) anasema kwamba mawasiliano yakiwa bora miongoni mwa mataifa, husaidia kuheshimu maamuzi ya watu wenye nia tofauti na hata ukubalifu wa misimamo tofauti ya watu hata kama haiko sawa na ya mwingine. Hii ina maana kwamba, mawasiliano bora husaidia kuwepo kwa maelewano. Kwa mujibu wa Conway (2011) na Lunenberg (2012) kufikia malengo na maono ya taifa fulani, kuna haja ya kuwepo na mawasiliano bora ambayo yatasaidia katika uwasilishaji wa hoja na malengo katika kipindi hicho. Hoja hii inatupa mwelekeo kwamba, ili kubadilisha mwanadamu ashike mwelekeo fulani, lazima kuwepo na mawasiliano bora na mawasiliano hayo yatawezesha kupitia kwa lugha.

Nchi nyingi za Afrika zinatumia lugha za kigeni kama vile, Kifaransa, Kijerumani na Kiingereza kama lugha rasmi. Hivyo, kuna haja ya kuwa na *Lingua Franca* ya mojawapo au baadhi ya lugha za kiafrika ambazo zimeimarika na zilizona wazungumzaji wengi kutumika kama lugha za mawasiliano miongoni mwa nchi wanachama Afrika na katika makundi ya kimakanda. Kiswahili ni miongoni mwa lugha kama hizi ambazo matumizi yake yamepita mipaka ya afrika mashariki na hata kutumiwa na mataifa mengine katika kanda nzima ya Afrika. Nchi nyingi Afrika hasa vyo, zinatoa mafunzo kwa wanafunzi wake katika kiwango cha Uzamili na Uzamifu. Japo wanafunzi hawa wanafanya utafiti kwa nia ya kukikua Kiswahili, haya yanabaki katika vitabu tu. Hata hivyo ni juhudi bora ambazo makala haya yanatilia mkazo kama juhudi za kupanua matumizi ya Kiswahili kama lugha yenye asili ya Kiafrika nje ya mipaka ya Afrika Mashariki.

Muungano ya Afrika (AU) umefanya juhudi pamoja na Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki ili kuimarisha matumizi ya Kiswahili Afrika. Chini ya Mwavuli wa “*Dares-Salaam Framework of Action*” inayoongozwa na “*African Academy of Languages (ACALAN)*”- Kitengo cha AU’s chenye lengo la kulinda na kuimarisha lugha za Kiafrika, Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki – KAKAMA – Kitengo cha Afrika Mashariki chenye majukumu ya kuimarisha na kuendeleza matumizi ya Kiswahili walikubaliana kushirikiana ili kukuza na kupanua matumizi ya Kiswahili Afrika Mashariki, katika Bara la Afrika na nje ya bara la Afrika. Hizi ni juhudi moja wapo mabazo nchi za Afrika zimekitambua Kiswahili kama lugha ambayo inauwezo wa kutumika katika mawasiliano katika bara nzima au kwa wanachama wengi wa AU hasa katika mikutano ya kikanda.

Katika mkutano uliolenga kukipigania Kiswahili kama lugha ya Kanda ya Afrika tarehe 26th-28th Juni, 2019, Dkt. Mwakyembe ambaye alikuwa Waziri wa Mawasiliano, Utamaduni, Sanaa na Michezo Tanzania wakati huo alihimiza haja ya mataifa ya Afrika na watu wenye asili ya Kiafrika kuungana. Alisema, Kiswahili kinatoa nafasi ya watu kujihisi kuwa na umoja na kujivunia kokote waliko kutokana na matumizi ya lugha yao ya asili. Dr. Mwakyembe alisema, kuna haja ya kukiimarisha na kukiendeleza Kiswahili kama azimio

la Afrika kwa kuleta umoja na maendeleo kama njia moja ya kukabiliana na mifumuko na utandawazi duniani. Wanasiasa pia wamekuwa mstari wa mbele hapa Afrika kukipigania na hata kukuza maendeleo ya Kiswahili hapa Afrika kama anavyoeleza katika Kamisheni ya Kiswahili Afrika mashariki Dkt. Simala. Dkt Simala anasisitiza kwamba Kiswahili ni Lugha ambayo inaleta umoja na maendeleo miongoni mwa watumiaji wake. Hivyo, aliunga mkono uamuzi wa AU wa kukitumia Kiswahili kama lingua franca ya Afrika katika azimio la Afrika na akahidi kushirikiana na AU katika kutumia Kiswahili kama kichocheo cha maendeleo na kufikia malengo ya AU.

Mwaka wa 2019 kama inavyoripotiwa na jaridi la “The Mast” nchi wanachama wa SADC zilikubaliana kutumia Kiswahili kama lugha rasmi miongoni mwa nchi zinazounda muungano huu. Baadhi ya nchi kwenye muungano huu ni Afrika Kusini, Angola, Botswana, Comoros, Democratic Republic of Congo, Eswatini, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Seychelles, Tanzania, Zambia and Zimbabwe. Kiswahili ni lugha Rasmi nchini Tanzania, Kenya na Rwanda na hivyo kuongezeka kwa nchi hizi pia ni hatua nzuri kwa lugha hii yenye asili ya Afrika. Hatua hii ya nchi wanachama kutambua Kiswahili kama lugha rasmi ilifanyika kwa sababu mbili. Kwanza waliteua Kiswahili ili kuenzi juhudi za Mwalimu Julius Nyerere na pili ni pia kuzipa lugha za Afrika hadhi ya juu kama zinavyopewa lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Kiswahili kuwa lugha yenye asili ya Afrika basi huenda ikapata hadhi ya juu Zaidi kuliko lugha hizi za kigeni. Aidha, Kiswahili pia kitakuwa kiunganisha cha mataifa haya ambayo mengi yana lugha tofauti tofauti zinazotumika kwao kulingana na wakoloni waliokuwa nchini mwao. Kama njia ya kuonyesha juhudi za Kiswahili, aliyekuwa rais wa Muungano wa Tanzania John Pombe Magufuli alitoa hotuba yake katika kikao hicho kwa lugha ya Kiswahili. Kama wanavyohoji Conway na Lunenberg, kuwepo na lugha ya kuwaunganisha watu waliona malengo na maono sawa ni hatua ya kupeleka mbele muungano huu na kwa kupitia lugha ya Kiswahili.

## **Kiswahili na Uchumi wa Afrika**

Kutokana na mjadala wa hapo juu, inabainika kwamba matumizi ya wingi lugha kwa maendeleo ya jamii ni

suala mjadala. Hata hivyo, kwa mujibu wa makala haya, wingi lugha hudidimiza maendeleo kiuchumi. Matumizi ya wingi lugha huleta tamaduni nyingi pamoja zenye matamano maono na maazimio tofauti. Na ili kufikia hatma ya malengo na azimio lao, kila jamii huwa na mfumo wake wa kimawazo ambao huigoza katika kufanya shughuli zao. Hivyo huku kunachangia kuimarika kwa ukabila miongoni mwa jamii. Watu hukosa kushirikiana kwa lengo la kujiamarisha kama kundi. Hata hivyo, inaonekana kwamba ili kuwepo na maendeleo yaliyoimarika na yenye mwelekeo stadi, yafaa mwasiliano yawe dhabiti na yenye mwelekeo mmoja. Lugha ndicho chombo ambacho hufanikisha mawasiliano. Mawasiliano bora huleta ushirikiano kutokana na watu au jamii hii kuwa na utamaduni sawa. Na kama anavyohoji Conway, mawasiliano bora huleta umoja katika taifa na hata katika jamii. Kuwepo kwa umoja kunarahisha ustawi wa kiuchumi na hivyo maendeleo ya uchumi.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Afrika ambazo zimepata ungwaji mkono mpana miongoni mwa mataifa ya Afrika kutumika kama *lingua franca*. Juhudi hizi zote zinafanywa ili kupata lugha ambayo ni yenye asili ya Kiafrika kando na lugha za kigeni ambazo zinatumika kama lugha za taifa katika mataifa mengi ya Afrika ili kutumika katika mawasiliano na katika makala haya tunasisitiza mawasiliano yakuleta maendeleo ya kiuchumi. Nchi wanachama wa SADC kwa mfano, walipopendekeza matumizi ya Kiswahili miongoni mwao kama moja wapo wa lugha ambazo zitatumika katika mikutano yao. Afrika Kusini imejitokeza kama nchi ya Kwanza katika muungano wa SADC kuanza kutoa mafunzo katika lugha ya Kiswahili ingawa somo lenyewe halijafanywa kuwa la lazima. Shule go kama inavyoripotiwa na gazeti la “*The East African*”. Aidha, Kiswahili ndio lugha ya kwanza ambayo asili yake ni ya nje ya mipaka ya taifa la Afrika Kusini kuwafunzwa shuleni. Hizi ni juhudi za kiwango cha juu cha kutafuta lugha yenye asili ya Kiafrika ambayo itatumika kuunganishi na lugha ya Mawasiliano miongoni mwa Waafrika.

## **MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Mahitimisho:** Hatua zinazochukulia na nchi za Afrika kutafuta lugha ya kutumika katika nchi zote Afrika ni juhudi za kupewa nguvu na kuungwa mkono na kila

nchi ya Afrika. Tunasema hivyo kutokana na msimo kwamba umoja katika lugha (Kiswahili) zitasaidia katika kukuza uchumi wa Afrika katika vitengo vyote vya biashara. Msimamo huu umechukuliwa mwanzo kutokana na juhudi za Muungano wa Afrika (AU) kukubali kushirikiana na Kamisheni ya Afrika Mashariki katika kukuza Kiswahili ili kutumiwe kama mojawapo wa lugha rasmi na kupewa hadhi sawa na Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani ambazo ni lugha za Kigeni. Pili, maendeleo hutegemea mawasiliano bora na ambayo

hufanikishwa na lugha. Kiswahili kuwa lugha yenye asili ya Kiafrika na juhudi hizi za maenezi kutoka kwa nchi za kiafrika basi itakuwa kiunganishi bora cha nchi hizi.

**Mapendekezo:** Hivyo tuwezeshe Kiswahili katika nyanja zote ili tufanikishe maendeleo ya Afrika. Tuishi siku zote tukikumbuka kwamba Umoja (wa lugha) ni nguvu, utengano ni udhaifu.

## MAREJELEO

- Alesina, A., & La Ferrara, E. (2005). Ethnic diversity and economic performance. *Journal of Economic Literature*, 43(3), 762–800.
- Conway, H. (1994). *Babel erased: The story of language and history*. Pentland.
- Easterly, W., & Levine, R. (1997). Africa's growth tragedy: Policies and ethnic divisions. *Quarterly Journal of Economics*, 112, 1203–1250.
- Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies*, 11(2), 185–197.
- Ku, H., & Zussman, A. (2008). *Lingua franca: The role of English in international trade* [Unpublished manuscript].
- Lian, B., & Oneal, J. R. (1997). Cultural diversity and economic development: A cross-national study of 98 countries, 1960–1985. *Economic Development and Cultural Change*, 46(1), 61–77.
- Lunenburg, F. C., & Ornstein, A. C. (2012). *Educational administration: Concepts and practices*. Wadsworth.
- Mkwinda, B. N. (2014). *Role of language in socio-economic development: The semiotics are right*.
- Noguer, M., & Siscart, M. (2003). *Language as a barrier to international trade? An empirical investigation* [Unpublished manuscript].
- Seargeant, P., & Erling, E. (2011). The discourse of English as a language for international development: Policy assumptions and practical challenges. In H. Coleman (Ed.), *Dreams and realities: Developing countries and the English language* (pp. 255–274). British Council.
- The Holy Bible: New International Version*. (1973).